# SHERIA YA KUTOZA KODI NA KUREKEBISHA BAADHI YA SHERIA ZA FEDHA NA KODI KUHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA SERIKALI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU


**VIFUNGU** **MAELEZO**

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI

1. Jina fupi na Kuanza Kutumika.
2. Marekebisho ya Sheria mbali mbali.

### SEHEMU YA PILI
### MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTARATIBU NA USIMAMIZI WA KODI NAM. 7 YA 2009

3. Kusomwa.
4. Marekebisho ya kifungu cha 3.
5. Marekebisho ya kifungu cha 23.
6. Marekebisho ya kifungu cha 40.
7. Kuongeza kifungu kipya cha 48A.
8. Kuongeza kifungu kipya cha 57A.
9. Kufuta na kuweka badala yake kifungu kipya cha 59.
10. Marekebisho ya kifungu cha 66.

### SEHEMU YA TATU
### MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHURU WA HOTELI NAM. 1 YA 1995

11. Kusomwa.
12. Marekebisho ya kifungu cha 3.
13. Kufuta Jadweli.

**SEHEMU YA NNE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA BODI YA MAPATO ZANZIBAR**
**NAM. 7 YA 1996**

14. Kusomwa.

15. Marekebisho ya kifungu cha 23.

**SEHEMU YA TANO**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA RUFAA ZA KODI ZANZIBAR**
**NAM. 1 YA 2006**

16. Kusomwa.

17. Marekebisho ya kifungu cha 27.

**SEHEMU YA SITA**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI NAM. 4 YA 1998**

18. Kusomwa.

19. Kufuta na kuweka badala yake kifungu kipya cha 3.

20. Kufuta kifungu cha 11A.

21. Marekebisho ya kifungu cha 16.

**SEHEMU YA SABA**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA ADA YA HUDUMA YA BANDARI, NAM. 2 YA 1999**

22. Kusomwa.

23. Kufuta na kuweka badala yake kifungu kipya cha 6.

**SEHEMU YA NANE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA, NAM 12 YA 2016**

24. Kusomwa.

25. Kufuta kichwa cha habari katika Sehemu ya Tisa na kuweka chengine badala yake.

## SEHEMU YA TISA
## "MFUMO WA UKUSANYAJI WA FEDHA ZA UMMA, UTARATIBU WA KIBENKI NA USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA"

26. Kuongeza kifungu cha 55A.

## SEHEMU YA TISA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAKAMPUNI NAM. 15 YA 2013

27. Kusomwa.

28. Kufuta na kuandika upya kifungu cha 82.

29. Marekebisho ya kifungu cha 238.

## SEHEMU YA KUMI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UHAULISHAJI WA ARDHI NAM. 8 YA 1994

30. Kusomwa.

31. Marekebisho ya kifungu cha 6.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHURU WA STEMPU NAM. 7 YA 2017

32. Kusomwa.

33. Marekebisho ya kifungu cha 60.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## MAREKEBISHO YA KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO NAM. 1 YA 2003

34. Kusomwa.

35. Marekebisho ya kifungu cha 4A.

**SHERIA NAM. 3 YA 2021**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

24 Juni, 2021

# SHERIA YA KUTOZA KODI NA KUREKEBISHA BAADHI YA SHERIA ZA FEDHA NA KODI KUHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA SERIKALI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na Kuanza Kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato), 2021 na itaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na Rais.

Marekebisho ya Sheria mbali mbali.

**2.** Sheria zilizotajwa katika sehemu mbali mbali za Sheria hii zinarekebishwa kwa namna zinavyoelezwa katika sehemu husika.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTARATIBU NA USIMAMIZI WA KODI NAM. 7 YA 2009

Kusomwa.

**3.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi Nam. 7 ya 2009, ambayo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**4.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingiza maneno mapya "mamlaka ya kodi ya kigeni" katika ufafanuzi kwa mpangilio wake wa kiherufi kama ifuatavyo:

"mamlaka ya kodi ya kigeni" maana yake ni Taasisi ya usimamizi ya kodi ya dola au nchi ambayo ina makubaliano na Zanzibar au Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kubadilishana taarifa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

Marekebisho ya kifungu cha 23.

**5.** Kifungu cha 23 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (6) kama ifuatavyo:

"(6) Mtu ambaye atashindwa kutoa stakabadhi au ankara ya malipo kama inavyohitajika chini ya kifungu hiki, atakuwa anatenda kosa na akitiwa hatiani atalipa kodi ambayo ilipaswa kulipwa pamoja na faini ya Shilingi za Kitanzania Milioni Mbili au asilimia Hamsini ya thamani ya kodi ambayo ilipaswa kulipwa kwa kila muamala ambao stakabadhi au ankara ya malipo haikutolewa yoyote itakayokuwa kubwa au kifungo kwa kipindi cha mwaka mmoja."

Marekebisho ya kifungu cha 40.

**6.** Kifungu cha 40 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta kifungu kidogo cha (2); na

(b) kukipa nambari upya kifungu kidogo cha (3) kuwa cha (2).

Kuongeza kifungu kipya cha 48A.

**7.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 48A mara baada ya kifungu cha 48 kama ifuatavyo:

Kubadilishana taarifa.

"48A. Kamishna anaweza kuomba kutoka au kubadilishana na mamlaka ya usimamizi wa kodi ya kigeni taarifa yoyote inayohusiana na mambo ya kodi ya mtu yeyote anaestahiki kutozwa kodi."

Kuongeza kifungu kipya cha 57A.

**8.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 57A mara baada ya kifungu cha 57 kama ifuatavyo:

Kutumia vibaya msamaha wa kodi.

"57A.-(1) Mtu ambaye amepewa msamaha wa kodi chini ya sheria yoyote ya kodi na akautumia vibaya msamaha huo, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika:

(a) kulipa kodi ambayo ingepaswa kulipwa endapo msamaha huo haukutolewa; na

(b) kulipa adhabu ya asilimia hamsini ya kodi ambayo ingepaswa kulipwa endapo msamaha huo haukutolewa.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hakutakuwa na msamaha wowote wa kodi utakaotolewa kwa mtu huyo".

Kufuta na kuweka badala yake kifungu kipya cha 59.

**9.** Kifungu cha 59 cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 59 kama ifuatavyo:

Uwezo wa Kamishna kukasimu.

"59.-(1) Kamishna anaweza, kwa kuzingatia masharti au mipaka yoyote ambayo anaona inafaa, kukasimu kwa afisa yeyote au mtu mwengine aliyeajiriwa kusimamia utekelezaji wa uwezo, kazi na majukumu aliyopewa chini ya Sheria hii.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Kamishna hatokasimu uwezo wa:

(a) kulimaliza kosa;

(b) kufunga sehemu ya biashara ya mtu anayepaswa kutozwa kodi; na

(c) kusamehe adhabu, faini au riba.

Marekebisho ya kifungu cha 66.

**10.** Kifungu cha 66 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuingiza maneno "barua pepe" baina ya maneno "posta" na "au" katika kifungu kidogo cha (1);

(b) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (3) mara baada ya kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

"(3) Upokeaji wa barua kwa njia ya kielektroniki utachukuliwa kwamba umefanyika wakati taarifa za kielektroniki zimetumwa kwa mtu anaejulikana au anuani iliyosajiliwa kielektroniki".

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHURU WA HOTELI
## NAM. 1 YA 1995

Kusomwa.

**11.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ushuru wa Hoteli Nam. 1 ya 1995, ambayo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**12.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (1) kama ifuatavyo:

"(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, kutawekwa tozo na kukusanywa ushuru unaojulikana kama ushuru wa hoteli kwa:

(a) muendeshaji wa hoteli, mkahawa na huduma nyengine za kitalii kwa kiwango cha asilimia kumi na mbili ya thamani ya huduma inayopaswa kutozwa kodi:

(b) mmiliki wa nyumba ya makaazi iliyokodishwa kupitia kwa utaratibu wa hoteli kupitia jukwaa la biashara mtandao au kwa njia nyengine kwa kiwango cha asilimia kumi na tano ya thamani ya ukodishwaji."

Kufuta Jadweli.

**13.** Jadweli la Sheria Mama linafutwa.

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA BODI YA MAPATO ZANZIBAR
## NAM. 7 YA 1996

Kusomwa.

**14.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria Bodi ya Mapato Zanzibar Nam. 7 ya 1996, ambayo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 23.

**15.** Kifungu cha 23 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (3) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (3) kama ifuatavyo:

"(3) Hesabu za mwaka za Bodi zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali."

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA RUFAA ZA KODI ZANZIBAR
## NAM. 1 YA 2006

Kusomwa.

**16.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Rufaa za Kodi Zanzibar Nam. 1 ya 2006, ambayo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 27.

**17.** Kifungu cha 27 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (1) kama ifuatavyo:

"(1) Bodi au Baraza, kama itakavyokuwa baada ya kuhitimisha usikilizaji wa mgogoro wa kodi, litatoa maamuzi yake kwa maandishi ndani ya siku sitini (60)".

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI NAM. 4 YA 1998

Kusomwa.

**18.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya 1998, ambayo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kufuta na kuweka badala yake kifungu kipya cha 3.

**19.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 3 kama ifuatavyo:

"3.-(1)Kutatozwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, kodi itakayojulikana kama "Kodi ya Ongezeko la Thamani" kuhusiana na usambazaji wa bidhaa au huduma Zanzibar na uingizwaji wa bidhaa na huduma Zanzibar kutoka eneo lolote nje ya Zanzibar.

(2) Endapo, kuhusiana na bidhaa zinazotozwa kodi, kodi imelipwa Tanzania Bara kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani inayotumika Tanzania Bara kwa kiwango sawa kama kinachotozwa Zanzibar, kodi itachukuliwa kwamba imelipwa kwa usambazaji unaotozwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii na hakuna kodi itakayolipwa kutokana na uingizwaji wake Zanzibar.

(3) Endapo, kuhusiana na bidhaa yoyote inayotozwa, kodi imelipwa Tanzania Bara kwa kiwango cha chini kuliko kinachotozwa Zanzibar chini ya Sheria hii, tafauti ya kodi itachukuliwa kuwa haikulipwa na italazimika kulipwa kwa uingizaji wa bidhaa hiyo Zanzibar kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

(4) Endapo, kuhusiana na bidhaa zozote zinazotozwa kodi, usambazaji umefanywa moja kwa moja na mtu anayepaswa kulipa kodi Zanzibar kumpelekea mtu aliyepo Tanzania Bara, Kamishna atakusanya kodi kwa niaba ya Tanzania Bara na ataiwasilisha kodi husika kwa Hazina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa kanuni zilizotungwa na Waziri."

Kufuta kifungu cha 11A.

**20.** Kifungu cha 11A cha Sheria Mama kinafutwa.

Marekebisho ya kifungu cha 16.

**21.** Kifungu cha 16 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongeza aya (e) mara baada ya aya (d) katika kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

"(e) kwa kuzingatia matakwa ya kifungu hiki, amelipa kodi kwa mtu anayestahiki kutozwa kodi Tanzania Bara kuhusiana na bidhaa yoyote inayotozwa kwa mujibu wa sheria inayotumika Tanzania Bara na kisha kuingiza bidhaa inayotozwa Zanzibar."

(b) kufuta neno "tatu" linalojitokeza baina ya maneno "ya" na "mfululizo" na kuweka badala yake neno "sita" katika kifungu kidogo cha (6).

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA ADA YA HUDUMA YA BANDARI, NAM. 2 YA 1999

Kusomwa.

**22.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ada ya Huduma ya Bandari, Nam. 2 ya 1999, ambayo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 6.

**23.** Kifungu cha 6 cha Sheria Mama kinafutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 6 kama ifuatavyo:

Uteuzi wa Mawakala

"6.-(1) Kwa madhumuni ya ukusanyaji wa tozo, Kamishna anaweza kuwateua watu wafuatao kuwa Mawakala wa ukusanyaji wa tozo na ataweka vigezo na masharti ya ukusanyaji huo:

(a) mtu ambaye anamiliki, anaendesha au anasimamia bandari kwa ajili ya bandari hiyo;

(b) mtu ambaye anamiliki, anaendesha au anasimamia utekelezaji wa usafiri wa anga au usafiri wa baharini kwa ajili ya utekelezaji huo;

(2) Kwa madhumuni ya kulinda maslahi ya ukusanyaji wa ada, Kamishna anaweza kumtaka Wakala aliyeteuliwa kulipa dhamana hiyo kama Kamishna atakavyoamua ambayo itataifishwa ikiwa Wakala ameshindwa kutimiza vigezo na masharti yaliyoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(3) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Kamishna anaweza, wakati wowote, kufuta uteuzi wa wakala iwapo ataona inafaa".

## SEHEMU YA NANE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA, NAM 12 YA 2016

Kusomwa.

**24.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016, ambayo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kufuta kichwa cha habari katika Sehemu ya Tisa na kuweka chengine badala yake.

**25.** Kichwa cha habari kilichopo katika Sehemu ya Tisa kinafutwa na kuweka badala yake kichwa cha habari kipya kama ifuatavyo:

**"SEHEMU YA TISA**
**MFUMO WA UKUSANYAJI WA FEDHA ZA UMMA, UTARATIBU WA KIBENKI NA USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA"**

Kuongeza kifungu cha 55A.

**26.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 55A mara baada ya kifungu cha 55 kama ifuatavyo:

Mfumo wa ukusanyaji wa fedha za umma.

**55A.**-(1) Fedha zote za Umma zitakusanywa kupitia mfumo wa malipo wa kielektroniki uliowekwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

(2) Afisa masuul atahakikisha fedha zote za umma zinakusanywa kupitia mfumo huo wa malipo wa kielektroniki kwa mujibu wa utaratibu ulioelezwa katika kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

## SEHEMU YA TISA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAKAMPUNI
## NAM. 15 YA 2013

Kusomwa.

**27.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Makampuni Nam. 15 ya 2013, ambayo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kufuta na kuandika upya kifungu cha 82.

**28.** Kifungu cha 82 cha Sheria Mama kinafutwa kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 82 kama ifuatavyo:

Kuwasilisha hati ya uhaulishaji na hati ya uthibitisho wa kodi.

"82.-(1) Bila ya kujali jambo lolote katika kanuni za kampuni, haitakuwa halali kwa kampuni kusajili uhaulishaji wa hisa au dhamana za kampuni isipokuwa hati stahiki ya uhaulishaji imewasilishwa kwa kampuni.

(2) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachoathiri uwezo wowote wa kampuni kusajili uhaulishaji kwa mmiliki wa hisa au mmiliki wa dhamana, au mtu yeyote ambaye anahaki ya hisa au dhamana za kampuni zilizohamishwa kwa utekelezaji wa sheria.

(3) Taarifa za mmiliki wa hisa au mmiliki wa dhamana zinazotokana na uhaulishaji wa hisa au dhamana hazitobadilishwa bila ya uwasilishaji wa cheti sahihi cha uthibitisho wa kodi kutoka Mamlaka ya Kodi kinachothibitisha kwamba kodi ya ongezeko la pato kwa mali za kudumu imelipwa au haipaswi kulipwa."

Marekebisho ya kifungu cha 238.

**29.** Kifungu cha 238 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (3) mara baada ya kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

"(3) Bila ya kujali masharti ya vifungu vidogo vya (1) na (2) vya kifungu hiki, kampuni iliyosajiliwa chini ya sheria zinazotumika Tanzania Bara itasajili kampuni tanzu ya kigeni chini ya sheria zinazotumika Zanzibar endapo **itafungua** biashara Zanzibar."

## SEHEMU YA KUMI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UHAULISHAJI WA ARDHI
## NAM. 8 YA 1994

Kusomwa.

**30.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Uhaulishaji wa Ardhi Nam. 8 ya 1994, ambayo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama."

Marekebisho ya kifungu cha 6.

**31.** Kifungu cha 6 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongeza aya mpya ya (j) mara baada ya aya (i) kama ifuatavyo:

"(j) cheti sahihi cha uthibitisho wa kodi kutoka mamlaka husika za kodi kinachothibitisha kwamba kodi ya ongezeko la pato imelipwa au haipaswi kulipwa".

(b) kuipa namba upya aya (j) kuwa (k).

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHURU WA STEMPU NAM. 7 YA 2017

Kusomwa.

**32.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam. 7 ya 2017, ambayo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama."

Marekebisho ya kifungu cha 60.

**33.** Kifungu cha 60 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta aya (b) na kuweka badala yake aya mpya ya (b) katika kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:

"(b) utaratibu wa mauzo ghafi ambao utajumuisha walipa kodi wote wanaotozwa kwa kiwango cha asilimia kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Nne la Sheria hii kwa kuzingatia kiwango cha asilimia mbili ya thamani ya usambazaji wa bidhaa na huduma zinazotozwa kodi."

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO, NAM. 1 YA 2003

Kusomwa.

**34.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo, Nam. 1 ya 2003, ambayo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama."

Marekebisho ya kifungu cha 4A.

**35.** Kifungu cha 4A cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (4) mara baada ya kifungu kidogo cha (3) kama ifuatavyo:

(4) Wakati wa kutekeleza uwezo chini ya kifungu hiki kuhusiana na utoaji au uingizaji wa bidhaa, KMKM itazingatia bidhaa zilizokatazwa, zilizozuiliwa na zilizodhibitiwa kwa mujibu wa Sheria ya Biashara Zanzibar.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 16 Juni, 2021.

.............................................
(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***